

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sitini na Moja – Tarehe 29 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo sasa aulize swali lake.

Na. 510

Barabara ya kutoka llembu hadi Itenka

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Barabara ya kutoka llembu hadi Itenka ni barabara muhimu kiuchumi.

Je, ni lini Serikali itafanyia ukarabati barabara hii?

Je, ni lini sasa Serikali itaweka hela ya kutosha kuhakikisha barabara hii inakwisha kabisa kwa sasbabu ni barabara hii ya kiuchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa sababu kalvati kutokana na mvua nydingi zinazonyesha, makalvati haya yanachukuliwa hatimae inakuwa siyo barabara ya kalvati tena yanakuwa madaraja, na mpaka sasa hivi tunasema tumetengeneza makalvati matano, na najua si muda mrefu makalvati haya yatachukuliwa na mvua.

Je ni lini Serikali sasa itatenga pesa za kutengeneza madaraja, yapo makalvati matano sasa yatatengenezwa madaraja matano, ni lini Serikali itatoa pesa?

NAIBI SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza alichokuwa anaomba kufahamu ni kwamba lini Serikali itatenga fedha za kutosha katika barabara hiyo ili kuhakikisha inakamilika?

Nimwambie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge Serikali tutaendelea kuzingatia hilo ombi alilolisema lakini kwa kadri ya bajeti yetu inavyoendelea kuongezeka ndivyo tunavyoendelea kutenda fedha za kutosha kwa ajili ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ilikuwa lini badala ya kujenga makalavati anataka tujenge madaraja katika eneo husika. Nimwambie tu kwamba sisi tunajenga kulingana na tathmini ambayo inafanywa na wakandarasi wa maeneo husika. Kwa hiyo, kama kutakuwa na hitaji la msingi la kujenga madaraja tutafanya hivyo baada ya

kufanya na kupata tathmini ya kina katika barabara hiyo kuhusu hayo makalavati anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Ummi Mwalim.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, na nataka kumpongeza Mheshimiwa Anna Lupembe kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, mpango wetu Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka 2022/2023 ni kujenga madaraja na makalvati yote, kwa hiyo, sasa hivi tumeshaelekeza *TARURA* katika Halmashauri zote kufanya usanifu, kazi inayofanyika sasa hivi ni usanifu wa madaraja na makalvati ili tuweze kujua gharama halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumeona tunaweze kutoa hela tukajenga barabara, lakini kama madaraja na makalvati hayajajengwa hayapitiki maana yake tumefanya kazi bure. Kwa hiyo kipaombele chetu sasa tunataka mwakani tukaelekeze kwenye madaraja na makalvati, kwa hiyo, niwatoe hofu tu waheshimiwa wabunge hili swala tumelipa kipaombele. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana, kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri amenifilisi, lengo langu lilikuwa ni suala la daraja kati ya Itenka na Kakese, na kwa kuwa fedha inakuja kutolewa nashukuru sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 511

Ujenzi wa Soko la Kisasa Tarime

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa ujenzi wa soko la kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Tarime wenye thamani ya shilingi bilioni 8.07 utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri. Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ilikidhi vigezo vya kupatiwa Shilingi bilioni 8.07 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa kupitia utaratibu wa Miradi ya Kimkakati mwezi Februari, 2019. Kutohana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi ya kimakatati Serikali ilisitisha baadhi ya miradi ya kimkakati iliyoindhinishwa ukiwemo mradi wa ujenzi wa soko la kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Tarime. Hata hivyo, Serikali imetoa kibali kwa Halmashauri ya Mji Tarime kuendelea na ujenzi wa Soko na katika mwaka wa fedha 2021/2022, shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko katika Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Tarime inatarajia kutangaza kazi ya ujenzi wa soko la kisasa mwezi Julai, 2021 na ujenzi unatarajiwaka kuanza mwezi Agosti, 2021 baada ya kumpata mkandarasi. Halmashauri imejipanga kukamilisha mradi huo ndani ya miezi 12 tangu tarehe ya kusaini mkataba.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko, swalii la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika nakuskuru. Mradi wa soko la Tarime ulikuwa uanze awali kama alivyosema February 2019 na wananchi wote waliokuwa na vibanda pale takriban 200 walibomolewa vibanda, kwa hiyo wamekuwa wakilipwa kwa muda huu wote, na majibu ya Serikali anasema utamalizika ndani ya miezi 12, na wametenda bilioni tatu tu, wakati mradi ni bilioni 8.07, ninependa kujua sasa hio bilioni 5.07 zinapatikana wapi ili ziweze kumalizika mradi huu ndani ya miezi 12 kama mlivyoonesha, maana yake mwaka wa fedha uko *within that?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, tuliweza kukidhi tena vigezo vya kupata stendi ya kimkakati ya Galamasara, na wananchi walikuwa wametoa takribani milioni 70 tangu mwaka 2017, ningependa kujua pia stendi hii ya kimkakati ya Galamasara ni lini inaenda kuanza na kumalizika? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kwa juhudii zake za kuunga mkono juhudii kubwa za Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Michael Kembaki katika kutetea wananchi wa Tarime Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nimhakikishie kwamba Serikali imeweka mpango wa kuhakikisha miradi mkakati ukiwemo ujenzi wa soko la kisasa katika Mji wa Tarime

unakamiliswa, na ndio maana katika mwaka wa fedha 2021/2022 tumetenga bilioni tatu na Serikali itaendelea kutenga fedha hizo kuhakikisha mradi huo unakamilika; pili fedha bilioni 5.07 zitawekwa kwenye mpango ujao wa fedha kuhakikisha linakamilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili *stand* hii ya kimkakati pia ni miongoni mwa mipango ambaeo Serikali itaendelea kuitekeleza kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, lengo la Serikali ni kuhakikisha miradi hii inakamilika na safari ni hatua, tunaanza na hatua moja tunakwenda kukamilisha hatua nyingine, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naamini kwa sababu mnao mpango wa kwenda miji mingi kujenga haya masoko na *stand*, ni vizuri tathmini ziwe zinafanywa na wataalamu yakajengwe zile sehemu ambazo wananchi wamezizoea, kwa sababu yakijengwa mbali sana wananchi wanapata changamoto kufika kwenye hayo maeneo, yanakaa majengo pale halafu watu hakuna, nadhani tunakuwa hatujatumia fedha za Serikali vizuri.

Tunaendelea na swali la Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Lungido, sasa aulize swali lake.

Na. 512

**Kumalizia ujenzi wa kipande cha Barabara ya
Sanya Juu kuelekea Kamwanga**

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa kipande cha barabara ya lami kilichoanzia Sanya Juu kuelekea Kamwanga ambayo kwa sasa imeishia Kijiji cha Elerai wakati zimebaki takribani kilometra 44 kuunganisha na kipande kingine cha lami kilichotoka Tarakea na kuishia Kijiji cha Kamwanga?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushkuru, kwa niaba ya Waziri Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu – Kamwanga yenye urefu wa kilometra 97.2 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami imekamilika. Ujenzi umepangwa kutekelezwa katika awamu tatu. Ujenzi katika awamu ya kwanza (*Lot 1*) wa sehemu ya Sanya Juu - Elerai kilometra 30.2 umekamilika. Serikali inatafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu ya pili (*Lot 2*) wa sehemu ya Elerai - Kamwanga kilometra 42 na awamu ya tatu (*Lot 3*) ya Bomang'ombe – Sanya Juu ambayo ni upanuzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali ikiendelea na juhudhi za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara tajwa, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 728.878 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, swali la nyongeza.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA Mheshimiwa Naibu Spika, nakuskuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswli madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii itakapokamilika itakuwa imekamilisha mzunguko wa Mlima Kilimanjaro kwa barabara ya lami, na hivyo itaongeza na kuchochaea kasi ya ukuaji wa

utallii wa Mlima Kilimanjaro na hifadhi ya Mlima Kilimanjaro vilevile. Kuna barabara nyengine ambayo ilipendekezwa kwenye llani tangu mwaka 2015, inayotoka Longido kuja kuungana na hii ya lami katika eneo la Sanya Juu, na barabara hii pia itapita ndani ya Hifadhi ya Jamii ya Indumet.

Je, Serikali imeweka mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hii ya kuunganisha hiyo Wilaya ya Longido na Mkoa wa Kilimanjaro na maeneo ya hifadhi na uzalishaji wa zao ya *West Kilimanjaro* inakwenda kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna barabara pia muhimu ya *TANROADS* inayotoka Longido mpaka Oldonyolengai mlima mwingine wa kitalii na maarufu duniani, pale ambapo itaungana na ile inayotoka Loliondo kuja mpaka Mto wa Mbu.

Je, Serikali itaanza lini kama ilivyo ahidiwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025 kufanya usanifu wa barabara ya lami kwa ajili ya barabara hiyo muhimu kwa biashara ya utallii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza ya Mheshimiwa Kiruswa, muhimu sana kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba wote kwamba ahadi zote ambazo zipo kwenye llani ya Uchaguzi za Chama cha Mapinduzi na zile ambazo zinazotolewa na viongozi wakuu wa Serikali zitatekelezwa kama zilivyopangwa, hiyo ni kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa naibu Spika, barabara mbili ambazo umezitaja zote ni muhimu sana, na unapojenga barabara

hizi, hii Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi unajua ni Wizara wezeshi, ukijenga barabara pale Mlima Kilimanjaro, utaongeza idadi ya watalii na mapato yataongezeka na utekelezaji wa llani utatekelezwa vizuri zaidi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nikwambie kwamba barabara ya Longido-Sanya Juu itaanza kujengwa kadri tukipata fedha pia Longido Oldonyolengai ambayo umeitaja nayo ni muhimu sana na tutaifanyia kazi, lakini nikupongeze kwa kazi unayoifanya ya kuwasemea wananchi wako wa Jimbo lako, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maganga swalii la nyongeza.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala liliopo Longido hata Mbogwe lipo; na ni mpango wa Serikali kila Halmashauri kuunganisha barabara za lami kwenda Makao Makuu ya Mkoa.

Je, Wizara inampango gani kulingana na Jimbo langu la Mbogwe sina barabara inayounganishwa Wilaya kwa Mkao? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhehimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba tumekuwa tukizungumza mara kwa mara kufatilia ujenzi katika jimbo lake na tumeshawaelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkao ili waangalie mipango iliyoko ndani ya mkoa wao, lakini pia tuangalie na hii ya Wizara. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango uliopo wa Serikali ni kuunganisha Mkao kwa Mkao, Wilaya na Mkao na Wilaya kwa Wilaya. Kwa hiyo hoja yako

tumeipokea Mheshimiwa Mbunge tutaifanyia kazi kadri ambavyo Serikali itapata fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa uliza swali lako.

Na. 513

Ujenzi wa Barabara ya Busega - Bariadi

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Nyashimo Wilayani Busega hadi Dutwa Wilayani Bariadi kupitia Shigala, Malili, Ngasamo na Imakanate yenye kilometra 47 kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nyashimo – Dutwa ni barabara ya Mkoa yenye ureu wa kilometra 47 inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyashimo – Dutwa ipo katika mpango mkakati wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 kwa ajili ya kufanyiwa upembizi yakinifu na usanifu wa kina. Barabara hii inaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali pamoja na ujenzi wa madaraja ili iweze kupitika majira yote ya mwaka

ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetengewa shilingi milioni 1,102.607 kwa ajili ya matengenezo pamoja na ujenzi wa Daraja la Shigala na la Malili. Ahsante,

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikupongeze wewe kwa kutaja jina langu vizuri na nimkumbushe tu Naibu Waziri, naitwa Simon Songe Lusengekile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara hii inachochea sana uchumi wa wananchi wa Jimbo la Busega na Jimbo la Bariadi, kwa maana ya Ngasamo, Shigara, Dutwa pamoja na Mariri.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu sana wa kuipa kipaombele barabara hii ili iweze kutengeneza kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tunaelekeea sasa mwisho wa Bunge letu la Bajeti; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kutembelea Jimbo la Busega ili aone umuhimu wa hii barabara? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhehimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lusengekile, Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana na ndiyo maana kwanza Mheshimiwa Mbunge tayari kuna fedha zipo anajengewa madaraja mawili hapa kama nilivyoyataja katika jimbo lake. Lakini, la pili tumeahidi kwenye jibu langu la msingi kwamba barabara hii inafanyiwa

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka huu wa fedha ambao unaanza Julai ambayo ni keshokutwa. Kwa hiyo, hii ikikamilika tutajenga barabara hii kwa kiwango cha lami tunajua umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili mimi niko tayari kufanya ziara kule Busega. Kwanza kuna shemeji yangu pale kwa hiyo nitaenda kumsalimia. Tuko tayari, tutaambatana. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu sasa aulize swali lake.

Na. 514

Ujenzi wa Barabara ya Kolandoto – *Oldean Junction*

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kolandoto – *Oldean Junction* utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Qangded – *Oldean Junction* yenye urefu wa kilometra 328 ni barabara kuu inayounganisha Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Singida na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 2,000 kwa

ajili ya kuanza ujenzi kwa awamu kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya barabara ya Kolandoto – Mwanhuzi yenyе urefu wa kilometa 62.5 na shilingi milioni 3,000 kwa ajili ya barabara ya Lalago – Ngóboko – Mwanhuzi yenyе urefu wa kilometa 74 ambayo ni sehemu ya barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Ujenzi wa barabara hizi utaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati juhudhi za kuanza ujenzi wa barabara hizo zikiendelea, Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo ya barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi milioni 849.97 zimetengwa kwa sehemu ya Kolandoto hadi Mwangongo mkoani Shinyanga, shilingi milioni 540.995 zimetengwa kwa sehemu ya Mwangongo hadi Sibiti mkoani Simiyu, shilingi milioni 579.118 zimetengwa kwa sehemu ya Sibiti hadi Matala mkoani Singida na shilingi milioni 1,507.352 zimetengwa kwa sehemu ya Matala hadi Oldean mkoani Arusha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya swali la nyongeza.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuonesha nia ya kuanza kujenga hii barabara kwa sababu ni ahadi ya muda mrefu iliyoko katika llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipande cha kilometa 74 ipo mito minne ya Itembe, Chobe, Lyusa na Nkoma ambayo imekuwa inakwamisha kuleta tija ya daraja la Sibiti lillilogharimu shilingi bilioni 34.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutembelea kipande hicho na kuweza kuishauri Serikali kuanza kujenga madaraja kwa fedha iliyotengwa mwaka huu wa fedha unaoanza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika barabara inayoiunganisha daraja la Sibiti kilometra 25 ambayo pia

imetengewa fedha iko juu ya mbuga kali sana. Kujenga barabara hii inatakiwa ianze katika kipindi cha kiangazi. Ni nini kauli ya Serikali kuhusu kuianza barabara hii kama ilivyotengewa fedha mwaka 2021/2022? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Leah Komanya kwamba yale ambayo tumejadili sana ulivyokuja ofisini bado yanabaki kuwa hivyo hivyo na nitaendelea kuyaeleza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Sibiti ambalo lina barabara ya maingilio yenye urefu wa kilometra 25 nataka nimhakikishie Mheshimiwa Komanya na wananchi wa Meatu kwamba tayari mkataba umeshasainiwa na muda wowote barabara yenye urefu wa kilometra 25 unaanza kujengwa, lakini hautajengwa kwamba ni kilometra nusu Simiyu na nusu Singida bali tutajenga zaidi upande wa Singida ambako ndiko kwenye bonde kubwa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika.

Kwa hiyo, tayari muda wowote barabara itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ambayo pia ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja aliyyataja naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Meatu niko tayari kwenda kuyakagua kwa sababu ni barabara ambayo imeongelewa sana, lakini nimhakikishie kwamba tayari tumeshafanya *design*, kwa hiyo, kinachotegemewa sasa hivi ni kupata fedha ili tutakapoanza ujenzi basi tutasubiri pia na tutategemea ushauri wake pengine ikiwezekana tuenze kwanza kujenga madaraja hayo

kabla ya kujenga barabara. Kwa hiyo, nitakuja kama alivyoshauri. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Venant Daudi Protas Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake.

Na. 515

Hitaji la Maji Safi na Salama - Igalula

MHE. VENANT D. PROTAS aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Kata za Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa uchimbaji wa mabwawa katika Kata za Mmale, Miswaki, Lutende na Kizengi ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imepanga kuboresha huduma ya maji kwenye Kata za Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo kuititia bomba kuu linalotoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Nzega, Igunga na Tabora.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa tenki lenye ujazo wa litu 1,000,000 na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometra 122. Mradi huu unatarajiwa kukamilika

kabla mwezi Juni, 2022 na utanufaisha wananchi wapatao 123,764 kwa kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 kukamilisha usanifu wa ujenzi wa bwawa katika Kata ya Kizengi na wakandarasi watapatikana mwezi Machi, 2022 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo ambapo wananchi wa Kata za Kizenga, Mmale, Miswaki na Lutende zaidi ya 60,000 watanufaika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venant Protas Daud, swali la nyongeza.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ulikuwa wananchi wa Kata za Goweko, Kigwa, Nsololo na Igalula kupata maji Desemba, 2021 lakini majibu ya Serikali yamekwenda tena Juni, 2022. Lakini utekelezaji wake mpaka sasa hivi umefikia asilimia 10.

Je, Serikali haioni kuusogeza karibu mradi huu uweze kutekelezeza kwa kasi ili wananchi wa kata hizo waweze kupata maji? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Jimbo la Igalula lina changamoto sana ya upatikanaji wa maji, ndio maana tunaelekeza Serikali iwekeze katika uchimbaji wa mabwawa. Niiombe Serikali haioni haja ya uharakishaji wa haraka wa usanifu wa uchimbaji wa mabwawa hasa hili Bwawa la Kizengi? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Igalula

kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Ni Mbunge mfuatiliaji, mpambanaji hususan katika suala zima la wananchi wake waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Nitoe shukrani kwa Bunge lako tukufu kwa kutuidhinishia fedha zaidi ya bilioni 680 lakini Mheshimiwa Rais naye ametupatia fedha ya nyongeza zaidi ya bilioni 207. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge maeneo ambayo tutayapa kipaumbele na kuyapa fedha za kutosha ili kukamilisha mradi ule ni eneo la mradi huu wa Igala kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wizara yetu ya maji tumeboresha Kitengo chetu cha Uchimbaji wa Mabwawa. Tunaona kabisa yapo maeneo ambayo hayana fursa ya uchimbaji wa visima. Tunataka maji ya mvua isiwe laana, tunataka tuyavune kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ili Watanzania waweze kunufaika na uvunaji wa maji ya mvua waweze kupata huduma ya maji.

Kwa hiyo, mkakati uliokuwepo tunakwenda kununua seti ya ujenzi wa mabwawa kwa maana ya vitendea kazi ili kazi hii ianze na Watanzania waweze kunufaika na ujenzi wa mabwawa. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Regina Qwaray swali la nyongeza.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona nami kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nishukuru Serikali kwa kuanzisha *RUWASA*, lakini pamoja na hayo *RUWASA* inakabiliwa sana na tatizo la upungufu wa wataalam pamoja na vitendea kazi.

Je, Serikali ina mkakati gani katika kutatua tatizo hilo ili kuleta ufanisi wa utendaji kazi? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maji. Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua umuhimu wa uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijiini - *RUWASA*; hili nipayekezo lenu Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, kikubwa ambacho tulianzisha *RUWASA* kwa minajimu ya kwenda kutatua tatizo la maji vijiini. Ipo changamoto hususan ya watumishi. Tumeomba kibali kupitia Ofisi ya Rais - Utumishi kuhakikisha kwamba tunapata watumishi wa kutosha. Lakini katika kipindi hiki maelekezo ambayo tumeyatoa Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba tuna Mamlaka za Maji kule mikoani waungane kwa pamoja ili katika kuhakikisha kwamba wana *team up* ili kuhakikisha kwamba miradi inakwenda na Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji katika Kata ya Mnazi, Tarafa ya Umba ni takribani miezi miwili sasa *RUWASA* wamepeleka saruji na mipira ile midogo, lakini mpaka sasa tunasubiri mabomba. Ni lini mabomba haya yatapelekwa ili maji katika Mji wa Mnazi na viunga vyake yaweze kupatikana kwa urahisi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Shangazi, kaka yangu ambaye anafanya kazi kubwa sana katika Jimbo lile la Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie maji hayana mbadala na sisi kama Wizara ya Maji umuhimu wetu na jukumu letu ni kuhakikisha tunalinda uhai wa wana Mlalo

na wana Mnazi. Natoa maelekezo kwa Mhandisi wa Maji wa pale Lushoto kuhakikisha mpaka Jumatatu mabomba yamefika na kazi ianze mara moja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu SPika, maji ni uhai kwa viumbi vyote, maji ni muhimu kwa ustawi.

Naomba kuuliza swali langu, Jimbo langu la Mchingga halina maji safi na salama. Sasa ningeomba jimbo hili lifikiriwe kwa umakini mkubwa kupata maji safi na salama kutoka chanzo kikubwa cha Ng'apa.

Je, ni lini maji safi na salama ya bomba yatapelekwa katika Jimbo langu la Mchingga kwa ajili ya wananchi wa jimbo hilo? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, dhati ya moyo kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mama yangu Salma Kikwete, kiukweli ni Mbunge ambaye kwanza anajua changamoto za watu wake na anaelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa. Kwa hiyo, naomba nimpe upendeleo maalum kabisa moja kufika kwanza katika jimbo lake la Mchingga, lakini la pili tunatambua kweli tuna chanzo toshelevu pale Ng'apa ambapo tumejenga mradi ule wa Lindi. Tunataka tuyatoe maji ya pale Ng'apa ili kuhakikisha kwamba yanafika katika Jimbo la Mchingga ili wananchi wa Mchingga waweze kuondokana na tatizo hilo la maji. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Ichemba lililopo katika Kata ya Ichemba likikuwa kwenye mpango wa upembizi yakinifu tangu mwaka 2015 lakini mpaka dakika hii halijawekwa kwenye huo mpango na baada ya kuingia RUWASA hilo bwawa limesahaulika kabisa. Tunajua bwawa hilo likikamilika linakwenda kutatua kero katika kata tisa za Jimbo la Ulyankulu.

Je, ni lini bwawa hili sasa litawekwa katika mpango wa upembizi yakinifu na kukamilika kwa ujenzi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze sana; katika kipindi ambacho tunaenda kuandika historia katika Wizara yetu ya Maji ni kipindi hiki kwa sababu Mheshimiwa Rais amedhamiria kwa dhati kabisa. Wanasema, yafaa nini imani bila matendo? Mheshimiwa Rais ametuongezea fedha zaidi ya shilingi bilioni 207 kwa ajili ya kwenda kutatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, maeneo ambayo tutawapa kipaumbele ni maeneo yale yenye changamoto na ninatambua Ulyanhulu ni maeneo ambayo yana changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaunga mkono na tutatoa fedha kuhakikisha ile kazi inaanza na wananchi wako waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephat Gwajima, swalii la nyongeza.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam kwenye Jimbo langu la Kawe hasa Kata ya Wazo kwenye eneo la Madale, Kisanga, Mbezi Juu hakuna maji kabisa. Waziri anasemaje kwa habari ya kuwapa maji watu wa Kawe, ni lini hasa Mheshimiwa Waziri? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, *brotherwangu Gwajima* kwa kazi kubwa ya muda mfupi ambayo anaifanya katika Jimbo lile la Kawe. Tarehe 5 Julai nitakuwepo Jijini Dar es Salaam nina mazungumzo na watu wa *DAWASA*.

Mheshimiwa Mbunge nikuombe uwepo katika kikao kile na moja ya maelekezo ya haraka tutakayoyafanya ni kuhakikisha wananchi wa Wazo wanaenda kupata maji kwa haraka. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Halima naona umesimama. Lakini Kawe mmealikwa kwenye kikao cha tarehe 5 Julai. Kwa hiyo, na wewe unaalikwa kwenye kikao cha tarehe 5 Julai.

Mheshimiwa Halima uliza swali lako kwa kifupi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za Serikali zinaonesha kwamba maji vijijini yanapatikana asilimia 74 na mijini ni asilimia 85 kwenda 90; lakini uhalsilia unaonesha kwamba mnasema watu wamepata maji kutokana na kuweka miundombinu na sio nyumba kwa nyumba.

Kwa kuwa sasa hivi tunaenda kwenye sensa ya Taifa ambapo watu wataenda kufanyiwa hesabu nyumba kwa nyumba. Kwa nini msitumie utaratibu huu wa sensa ili kuweza

kupata takwimu halisi ya kila nyumba ambayo inapata maji nchi hii? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze na nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge dada yangu Halima, sisi Wizara yetu ya Maji inafanya mageuzi makubwa sana na moja ya eneo ambalo eneo unalizingumzia sisi tumeshalifanya kazi. Tumekutana na watu wetu wa takwimu ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye hilo hilo. Lakini tunataka tujiongeze mbali zaidi. Badala ya kusema tu asilimia ngapi watu wanapata maji, tunataka twende mbali zaidi, tunataka tujue Tanzania kuna vijiji vingapi, vingapi vimepata maji, vipi havijapata maji ili tuhakikishe tunaviongezea nguvu maeneo ambayo hayana maji ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 516

Mikakati ya Uzalishaji Kiwanda cha Man'gula

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanza uzalishaji katika Kiwanda cha Chuma Mang'ula?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uchumi wa viwanda hapa nchini, pamoja na mambo mengine unalenga kufufua na kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mang'ula Mechanical Workshop* ni karakana iliyoanzishwa kwa msaada wa Serikali ya China mwaka 1969. Karakana hiyo ilianzishwa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa vipuri mbalimbali ya mitambo iliyokuwa inatumika wakati wa ujenzi wa Reli ya Tanzania-Zambia (TAZARA), pamoja na utengenezaji wa vipuri sehemu ya eneo la karakana hiyo ilitumika kujenga kiwanga cha *Pre-Fabricated Concrete Manufacturing* kwa ajili ya kutengeneza mataruma ya zege kwa maana ya *concrete slippers* na nguzo za zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, karakana ya *Mang'ula Mechanical and Machine Tools Company Limited* ilirejeshwa Serikalini mwaka 2019 kutokana na mwekezaji wake kushindwa kuendeleza kiwanda hicho kwa mujibu wa mkataba wa mauziano. Kufuatia urejeshwaji huo Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Msajili wa Hazina imeandaa utaratibu wa kutafuta wawekezaji wapya watakaoviendesha viwanda hivyo kikiwemo kiwanda cha *Mang'ula Machine and Mechanical Tools Limited*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Asenga swalii la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, japo kuwa majibu ya Serikali zijaridhika nayo sana, lakini kwa kuzingatia kuwa Kassim Faya Nakapala Mwenyekiti wa Halmashauri na Ebeneza Emmanuel Katibu wa CCM wa Wilaya wako hapa kufuatilia mionganini mwa mambo mengine jambo hili na Diwani wa Kata husika Fatma Mahigi wa Mang'ula "B" kwamba eneo hili sasa limekuwa hatarishi sana ni eneo ambalo lina ekari takribani 250 na akina mama

wameshaanza kubakwa. Naomba kuiuliza Serikali maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza Serikali ipo tayari kuweka ulinzi wakati huu inatafuta mwekezaji wa kuwekeza katika Kiwanda hiki cha *Machine Tools*?

Lakini pili naomba kuiuliza Serikali sasa hivi tunajenga reli ya kisasa ya *SGR* na hii reli ya kisasa itahitaji mataruma na kadhalika, kwa nini wasikabidhi eneo hili na kiwanda hiki kwa *SGR* ili iendelee kutumia kuzalisha vifaa vya reli? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Asenga kwa ufuatiliaji kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo lake na hasa katika sekta ya viwanda na kwa ajili ya ufufuaji wa kiwanda hiki cha *Mang'ula Machine Tools*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli eneo hili limekuwa kwa muda mrefu halitumiki kama nilivyosema kwa sababu mwekezaji aliyepewa eneo hili kuliendeleza hajaliendeleza kwa muda mrefu, nichukue nafasi hii kumuahidi kwamba tutashirikiana na Halmashauri kuona namna bora ya kuweka ulinzi ili eneo hili lisiwe hararishi kwa sasa ambapo bado hatujapata mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili kama nilivyosema tunaangalia matumizi bora ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji ambao wataweza kutumia eneo hili kwa ajili ya kuwekeza viwanda, tuchukue pia hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba kama wenzetu wa reli ya

kisasa watataka kutumia eneo hili kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kutumika katika *SGR* basi nao tutawakaribisha, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kiwanda hiki kipo katika eneo la kimkakati kwa sababu kimezungukwa na mashamba ya miwa ama eneo ambalo linalima miwa kwa wingi, na kwa kuwa kulikuwa na mpango wa ku-*transform* kiwanda hiki kwenda kuzalisha sukari.

Je, Serikali inatoa tamko gani ikizingatiwa kwamba sasa hivi kuna mpango wa kuboresha viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha sukari?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukanda huu wa Kilombero ni ukanda ambao tunaweza tukasema ni wa kimkakati kwa uzalishaji wa miwa na sukari kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya hapa nchini. Ni kweli ni moja ya azma ya Serikali kuhamasisha au kuvutia wawekezaji wengi katika kuchakata miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema katika jibu la msingi tunatafuta wawekezaji mahiri ambao watajitokeza kuwekeza katika eneo hili ikiwemo wale ambao watataka kuchakata miwa basi na sisi tutawakaribisha ili

kutumia nafasi hiyo katika eneo hili la *Machine Tools* kama sehemu ya kuwekeza viwanda vya kuchakata miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tupo tayari na tusaidiane na Wabunge ili tuweze kuwekeza katika maeneo haya kwa umahiri zaidi, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 517

Mpango wa kukarabati Hospitali ya Mkoa wa Mtwara

MHE. HASSAN S. MTENGA aliuliza:-

Majengo mengi katika Hospitali ya Mkoa wa Mtwara yamechakaa; je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara - Ligula ni moja kati ya Hospitali za muda mrefu hapa nchini ambazo miundombinu yake imechakaa sana. Katika jitihada za kuboresha miundombinu ya Hospitali hiyo, kwenye bajeti ya 2020/2021 kiasi cha shilingi milioni 201 kimetolewa kwa ajili ya ukamilishwaji wa jengo la kuhifadhi

maiti ambalo ujenzi wake umekamilika na vifaa vimenunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi bilioni moja kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Majengo ya Wagonjwa wa Nje (*OPD*), wodi za wanaume na wanawake, upasuaji, wodi ya uangalizi maalum na kichomea taka. Ukarabati huo unatarajiwa kukamilika Machi, 2022. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa hospitali ile ni kongwe na mpaka sasa hivi kwenye Hospitali ya Ligula Mtwara haina *x-ray machine*, lakini katika suala hilo la kutokuwa na *x-ray machine* huduma za *theatre* kwa ujumla wake hazipo.

Je, ni lini Serikali sasa itaamua kututengenezea masuala mazima ambayo yanahusu *package* hiyo ya *x-ray machine* pamoja na jengo la *theatre*? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, je, ni lini Serikali itaratibu suala zima la kutuletea Madaktari Bingwa ambapo tunashida ya Madaktari Bingwa wa Watoto, Madaktari Bingwa wa Koo ambao vifo vinasababisha kuwa vikubwa sana kwenye hospitali yetu? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Hassan Tenga kwa ufuatiliaji wake wa kina sana kwa suala zima la Hospitali ya Mkoa, lakini sio tu

Hospitali ya Mkoa, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwenye Wilaya yake.

Swali lake la kwanza ni lini hospitali hiyo itapata *x-ray*, lakini pamoja na vifaa vya *theatre*. Kama ambavyo nimekuwa nikisema hapa Rais wetu miezi michache iliyopita alitoa shilingi billioni 123 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na dawa na hospitali yake hiyo ipo kwenye bajeti kwa ajili ya vifaa husika ambavyo ameulizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili analoulizia ni suala ambalo mimi na yeze kama ambavyo nimemuomba la madaktari kupelekwa kwenye hospitali yake; na ni ukweli kwamba kuna tatizo la madaktari kwenye maeneo mengi tu sio eneo la kwake na kuna makakati huo sasa wa ajira mpya ambazo zinakuja tunamfikiria lakini mimi na yeze kama tulivyopanga tutakwenda kwenye hospitali yake kufuatilia Hospitali ya Mkoa tutakwenda pamoja tutaona tatizo ni kubwa kiasi gani tuone tunafanya nini kuhamisha sehemu nyingine ili madaktari waweze kusaidia eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize Hospitali ya Wilaya ya Hai imekuwa na changamoto kubwa sana ya majengo mpaka ninivyozungumza hatuna jengo la mama na mtoto, hatuna jengo la *pharmacy*, hatujaa jengo la maabara kakini pia *work way* za kuwasiliana kwenye majengo haya hatuna.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea majengo haya? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kaka yangu Saashisha Mafuwe kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwenye Wilaya ya Hai hasa kwenye kufuatalia miundombinu tu sio tu ya Hospitali ya Wilaya, lakini zahanati zake lakini vituo vya afya na Hospitali ya Machame ambayo ni *DDH*, ni ya kanisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kuna kazi kubwa sana inafanywa na Waziri wa Afya Mheshimiwa Dorothy Gwajima pamoja na Waziri wa TAMISEMI dada yetu Ummy Mwalimu ya kuhakikisha tunapata *resources* kupita *sources* zingine ili tuweze kukamilisha miradi kama hiyo ambayo anaisema ambayo inawezekana haijaingia kwenye bajeti kubwa ambayo sasa tumeipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Saashisha tukitoka hapa twende pamoja, tuangalie mkakati huo wa Mawaziri wetu wawili tuone ni namna gani inaweza kufanyika kupitia *Global Fund*, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana; kwa kuwa Serikali imeendelea na ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mandewa, nataka kujua tu ni nili itakamilisha ukarabati huo ili kuondoa adha inayojitokeza katika suala la kupata huduma ya afya katika Mkoa wa Singida? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tulishakwisha kusema hapa kwa bajeti ya mwaka 2021/2022 zimetengwa zaidi ya shilingi bilioni 57 kwa ajili ya kufanya ukarabati na

ujenzi katika hospitali mbalimbali za rufaa hapa nchini hospitali aliyoitaja Mheshimiwa hapa ni mojawapo ya hospitali ambayo ipo kwenye mpango huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Hospitali ya Rufaa ya Ligula tuna ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara ambao naishukuru Serikali imekamilisha kwa awamu ya kwanza; je, Serikali imejipangaje kuanza ujenzi awamu ya pili ya hospitali hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo amekuwa karibu sana kufuatilia ujenzi wa Hospitali hiyo ya Rufaa ya Kanda nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwenye bajeti ya mwaka huu ni moja wapo ya hospitali ambazo zimetengewa fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na kumalizia baadhi ya *unit* ambazo ilikuwa hazijamaliziwa, ni hospitali aliyoitaja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *x-ray* katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Ligula mimi niliuliza hilo swali Bunge liliolopita Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Ndugulile aliniambie *x-ray machine* ya Mkoa wa Mtwara ipo bandarini, leo majibu ya Naibu Waziri anaongea *as if* hakuja kitu kabisa.

Mimi nataka tu kujua ile x-ray yetu ambayo tuliambiwa ipo bandarini ime-*evaporate* au vipi? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze dada yangu mpambanaji kwa swali lake zuri ambalo linahusu wananchi; moja ni kwamba anasema kwamba *x-ray* hiyo ilikuwa ipo bandarini na mpaka sasa haijafika kwenye eneo husika. Nikuombe dada yangu tukimaliza maswali hapa twende mimi na wewe tukakae pale tufuatilie hiyo *x-ray* na tuweke utaratibu iweze kufika mapema inapotakiwa, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Wizara ya fedha na Mipango, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 518

Shirika la Bima la Zanzibar

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: aliuliza:-

Kumekuwa na kawaida kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kutotumia huduma za Shirika la Bima la Zanzibar kwa kisingizio kuwa shirika hilo siyo la umma.

(a) Je, Serikali inalitambua shirika hilo kama la Serikali au shirika binafsi?

(b) Kama ni shirika la Serikali, mini wito wa Serikali kwa watendaji ambao wamekuwa wakikataa kutumia huduma hiyo kwa kisingizio cha kuwa siyo shirika la Serikali?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Chande majibu kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar yaani *Zanzibar Insurance Corporation* limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009 na lina leseni hai yenye usajili Na.00000704 inayoruhusu Shirika hilo kufanya biashara ya bima za kawaida yaani *Non-Life Insurance*. Shirika hilo linamiliikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwa shirika hilo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sio Shirika binafsi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shirika la Bima la Zanzibar ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wito wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa watendaji ambao wamekuwa wakikataa kutumia huduma zake kuendelea kulitumia shirika hilo kwa ajili ya kupata huduma za bima kama ambavyo wanalitumia Shirika la Bima la Taifa hasa ukizingatia kuwa biashara ya bima nchini ni biashara Huru na Huria inayosimamiwa na Sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009 pamoja na Kanuni zake. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swalii la nyongeza.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naishukuru Serikali kuitia kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Muungano kwa niaba ya Waziri wa Fedha kwa majibu mazuri ambayo nafikiri sasa yataielekeza nchi yetu kuwa shirika hili ni la Serikali kwa mujibu wa sheria.

Swali langu ni moja tu kwamba kwa vile Serikali imeelekeza taasisi za Muungano na taasisi zote za Serikali

kutumia Shirika la Bima la Taifa sasa kwa nini Serikali hairudi na kuelekeza wananchi wake ili waelewe kwamba Shirika la Bima la Zanzibar ni Shirika la Kiserikali na wana wajibu pia wa kutumia kulingana na huduma zao wanakavyoona ni nzuri na mimi nikiwathibitishia wabunge kwamba huduma hizo ni nzuri? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira - Mheshimiwa Hamad Chande kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Najma kwa juhudini yake ya ufuatiliaji wa kero za wananchi na kwa namna anavyopambana kwa wananchi wote, kwa kweli naomba hili tulichukue kama ni wazo, ni ushauri na tutalifanyia kazi. Tutashauriana na Serikali kulifanyia kazi jambo hili, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwa Wabunge, lakini majibu kutoka upande wa Serikali na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele.

Kwanza ni tangazo la wageni; tutaanza na wageni walipo jukwaa la Mheshimiwa Spika, nao ni wageni saba wa Mheshimiwa Spika kutoka Benki ya Exim ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Matawi Ndugu Agness Kaganda, karibu sana. (*Makofi*)

Lakini Ndugu Agness Kaganda ameongozana na wafanyakazi wengine mmoja ni Rose Kubagwa, karibu sana; Edina Abraham, karibu sana; Anitha Goshashy, Chiku Chambuso, Glynis Stambuli, George Kiluvia, Ramadhani Magera. Huko Exim inaonekana akinamama wametia for a, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Lakini pia wapo wageni watatu wa Katibu wa Bunge kutoka Kampuni ya DSTV ya Jijini Dar es Salaam ambao ni

Meneja wa Kanda Ndugu John Kichele, Afisa Mauzo Ndugu Octavian Minja na Ndugu Vitus Ugulumu, sijui wamekaa upande gani hao, karibuni sana wageni kutoka DSTV. (*Makof*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi ambao ni familia yake kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na mke wake Ndugu Esther Ndakidemi, karibuni sana familia ya Profesa Ndakidemi. Esther ndio yupi hapo jamani? Karibu sana shemeji na wifi yetu. (*Makof*)

Wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni 30 wa Mheshimiwa Angeline Mabula - Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Kituo cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana cha A/CT Jimbo la Ilemela Mkoani Mwanza wakiongozwa na Mchungaji Zephania Masaga, karibuni sana vijana na Mchungaji kutoka Ilemela. (*Makof*)

Lakini pia wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye ni Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na hawa ni viongozi wa KKKT Kwaya ya Elitegemeo kutoka Jimbo la Babati, Mkoani Manyara wakiongozwa na Mchungaji Witness Nadeiti, karibuni sana. Mchungaji Nadeiti ndio yupi hapo? Jamani Mchungaji mwanamama huyu, karibu sana. (*Makof*)

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mwita Waitara - Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni viongozi wa CCM kutoka Wilayani Tarime wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya Ndugu Hamis Mkaruka, karibuni sana viongozi wetu kutoka Tarime. (*Makof*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia nao ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya ya Mafia, Mkoani wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Mohamed Faki, karibuni sana. wajumbe hawa jamani naona

walimtendea haki kabisa Mheshimiwa Omari Kipanga, kwa hiyo hawa si sehemu ya wale wajumbe wengine. (*Makofi*)

Lakini wapo pia wageni 31 wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Jimbo la Kilombero, Mkoani Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Kassim Nakapala, karibuni sana viongozi wetu na Madiwani wetu, nadhani mmemuona Mheshimiwa Mbunge anavyofanyakazi nzuri. (*Makofi*)

Wapo pia wageni 10 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Ikungi, Mkoani Singida wakiongozwa na Ndugu Kilimbinda Sawia, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambao ni familia yake kutoka Chunya, Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Ndugu Malcom Kasaka, karibuni sana. Sasa hapa sijatajija wale kama wote ni watoto wa Mheshimiwa Kasaka ama wengine ni namna gani, lakini hebu simameni tena maana nimeambiwa wanaongozwa na Malcom Kasaka, kwa hiyo mmoja wapo hapo ndiyo Malcom Kasaka wengine wote wanafuata na wenyewe, umefanyakazi nzuri Mheshimiwa Mbunge naona mambo mazuri. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Ahnaf Mohamed na Ndugu Said Aman, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawaona kuna Wabunge wanapirika humu ndani wanaendelea kuzunguka, wengine wako wanaongea, sijui wamesahau nimesimama hapa mbele, nasoma huku nawaona, nitaanza kutaja mmoja mmoja na wengine hawana hata habari ya ninachosema hapa mbele wanaendelea kuongea na mwingine ndiyo kwanza kasimama anataka kutembea. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kila siku nikiwa nimesimama hapa mbele inabidi msubiri nikae, maana unawenza kuwa wewe ndiyo unaongelewa habari zako hapa mbele, halafu wewe unaongea na Mbunge mwenzio. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange ambaao ni familia yake kutoka Mbezi. Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wake Ndugu Alafisa Dugange, karibuni sana. Alafisa Dugange ndiyo yupi kati yenu? Jamani wifi yetu na shemeji yetu, karibu sana. Naona vigelegele hapa vimeongezeka. (*Makofi*)

Lakini tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaao ni Kwaya ya Chuo Kikuu cha Dodoma UDOM wakiongozwa na Mchungaji Keneth Masaka, nafikiri wameingia, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ritta Kabati anaye mgeni mwingine ambaye ni Ndugu Frank Nicholaus kutoka Chuo cha Diplomasia Kurasini, Jijini Dar es Salaam karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Irene Ndyamukama ambaao ni wanakwaya kutoka Kanisa la Mlima wa Moto wa Bwana la Jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji naona jina lake halijawekwa hapa. Wageni wa Mheshimiwa Irene Ndyamukama haya nafikiri hawakupata fursa..., Aah, wako upande huu, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 68 wa Mheshimiwa JaneJelly Ntate ambaao ni wana maombi wa mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Isaya Njendaluzi, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Lakini pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jonas Zeeland ambaye ni Diwani kutoka Mvomero, Mkoani Morogoro na huyu ni Mheshimiwa Coster Reuben, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Tunza Malapo ambaao ni Ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Dkt. Shakeel Saleem, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea ambaao wanatoka Accra, Ghana na hawa ni Askofu Oral Justice, Mchungaji Ambwene Kilujenga na Mchungaji Noble, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Protas ambaao ni rafiki zake kutoka Jimboni Igalula, Mkoani Tabora na hawa ni Ndugu Rashid Kaombwe na Ndugu Joseph Bicha, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambaao ni marafiki zake kutoka Ukonga, Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Diana Laizer, Ndugu Mwasi Masanyiwa na Ndugu Shafii Mzobora, karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Sasa Mheshimiwa Jerry Silaa alikuwa anaeleza hapa huyu Diana, Diana ndiyo yupi katika hao huyu Diana naona Mheshimiwa Ritta Kabati alikuwa ana kicheko fulani hivi, lakini huyu Diana Simon Laizer yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *Lavin International Agency Ltd.* ambaao hawa ndiyo waandaaji wa zile tuzo maarufu kabisa tunazozifahamu za *Consumer Choices Awards*. (*Makof*)

Kwa hiyo, Diana pamoja na wenzake tunawapongeza kwa ubunifu wenu na sasa badala ya kufanya tu Tanzania taarifa zilizopo wanataka kuifanya *Consumer Choices Awards Africa* na huyu ni Mtanzania ambaye anaenda kutangaza mambo mazuri huko wameshatoa hizi awards mara nyingi kwa miaka miwili mfululizo na sasa wanaenda Rwanda, Nigeria na Afrika Kusini na Mheshimiwa Jerry Silaa ni Mjumbe wa Bodi ya *Lavin International*. (*Makof*)

Kwa hiyo tunawapongeza sana Diana pamoja na wenzako kwa ubunifu huo na wengine waige mfano huo wa

kuwa wabunifu wa mambo mbalimbali si lazima kile kile anachofanya Diana, lakini tunawatia moyo wabuni mambo mengine ambayo na wao yatawasaidia kufanyakazi vizuri. (*Makofi*)

Tunao wageni 60 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Kanisa la Moravian Jimbo la Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Felix Mwasongwe, wako upande gani hawa? Karibuni sana, karibuni Bungeni. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambaao ni wapiga kura wake kutoka Babati, Mkoa wa Manyara na hawa ni Ndugu Simon Bajuta na Elias Shingat karibuni sana. Pia tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Elibariki Kingu ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Swabrina Mpondoo, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 90 kutoka Shule ya Msingi El-Shaddai ya Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanyakazi na kuendesha shughuli zake na hawa wameongozwa na Mwalimu Isaack, karibuni sana Bungeni, tunaamini mmeweza kujifunza mambo mbalimbali kwa siku ya leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine linalotoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Spika ameridhia kuanzisha Kikundi cha Vinara wa Elimu bora Bungeni. Sasa hapa naona kimeandikwa aidha ni PAJEA au PAKEA. (*Makofi*)

Haya naambiwa kinaitwa PAKEA, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge baada ya kuahirisha shughuli hizi Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba muonane kwa kifupi sasa hapa hajasema muonane wapi lakini nadhani mkitokea kwenye lango kuu basi mtamkuta pale atawapa maelezo wapi muweze kuonana. (*Makofi*)

Hapa nimeletewa tangazo lingine la mgeni mwiningine wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na huyu ni Mheshimiwa ama alikuwa Mheshimiwa ama bado ni Mheshimiwa Bungara sijui yuko wapi. Jamani huyu ni Mheshimiwa alikuwa Mbunge katika Bunge liliopita. (*Makofi/Vigelegele*)

MBUNGE FULANI: Tunaanza upya.

NAIBU SPIKA: Ngoja sasa ili mpige makofi vizuri tusikilizane kidogo. Mheshimiwa Bungara alikuwa Mbunge hapa Bunge liliopita na huko nyuma, lakini pia huyu ni maarufu kwa jina la Bwege. (*Makofi/Vigelegele*)

Sasa kuna wakati wananchi walipata wakati mgumu wakifikiri alivyoitwa Bwege alikuwa ametukanwa kwamba ye ye ni bwege, lakini kumbe ni jina lake anaitwa pia Bwege na ni maarufu kwa kweli, sitaki kuirudia ile misemo yake hapa maana siahirisha Bunge bado, lakini Mheshimiwa Bwege tumefurahi sana kukuona tena na karibu Bungeni na kama unavyoona kwenye kiti chako naona amekaa Mheshimiwa Aleksia kwa wale ambao hawafahamu Mheshimiwa Aleksia hicho ndiyo kiti alikuwa anakaa Mheshimiwa Bwege. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwa hiyo, tunajifunza tu kwamba tujitahidi kutunza vile viti vyetu maana unaweza ukasukumwa ukajikuta umekaa kule juu siku nyingine ukija humu ndani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana na baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, eti hawez? (*Kicheko*)

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Jifunze kanuni.

(*Saa 4.20 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 30 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi*)